
# TAJIRI NA LAZARO

Somo la 14



Neno lako ni kweli – Yohana 17:17

*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# TAJIRI NA LAZARO

Hapo awali tulijifunza kutoka katika Maandiko kwamba nafsi inaweza kuharibiwa na kwamba inakufa. Pia tulijifunza kwamba wanadamu hawana nafsi bali wao **ni** nafsi. Kwa hiyo tunapokufa, nafsi zetu [ikimaanisha sisi wenyewe] ndizo hufa: *"Wote washukao mavumbini watamsujudia, wala **hakuna awezaye kuiweka hai nafsi yake**"* (Zaburi 22:29, *KJV*).

Tulijifunza mistari ya Biblia iliyoonekana kupingana isipokuwa kwa mfano mmoja, Tajiri na Lazaro. Hivi ndivyo Yesu alisema:

*"Palikuwa na tajiri mmoja aliyevaa nguo za zambarau na kitani safi na kuishi maisha ya starehe kila siku. Mlangoni mwake palikuwa na ombaomba(maskini) mmoja aitwaye Lazaro, ambaye ana vidonda na akitamani kula kile kilichoanguka kutoka kwenye meza ya yule tajiri. Hata mbwa walikuja na kulamba vidonda vyake. Wakati ulifika ambapo yule ombaomba alikufa na malaika wakamchukua mpaka kifuani mwa Abrahamu. Yule tajiri naye akafa akazikwa. kule kuzimu, mahali alipokuwa katika mateso, alitazama juu, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro karibu naye. Basi akamwita, Baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu, kwa maana ninateseka katika moto huu. Lakini Ibrahimu akamjibu, Mwanangu, kumbuka ya kuwa ulipokea mema yako katika maisha yako, na Lazaro alipata mabaya, lakini sasa yeye anafarijiwa hapa, na wewe unateseka. Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale wanaotaka kutoka huku kwenda kwenu wasiweze, wala mtu yeyote kutoka huko asiweze kuvuka kuja kwetu. Akajibu, basi, baba, nakuomba, umtume Lazaro*

*nyumbani kwa baba yangu, maana ninao ndugu watano. Na awaonye, ili wao pia wasije mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akajibu, Wana Musa na Manabii; waache wawasikilize. Akasema, la, baba Ibrahimu, lakini ikiwa mtu kutoka kwa wafu akiwaendea, watatubu. Akamwambia, wasipowasikiliza Musa na manabii, hawatasadiki hata akifufuka mtu katika wafu."* (Luka 16:19-31[1])

Baadhi ya Wakristo wanaamini kwamba maneno haya yanafundisha mafundisho mawili: 1) fundisho la kutokufa, yaani asili ya kutokufa kwa nafsi baada ya mauti; na 2) fundisho la kuwako kwa kuzimu kama mahali pa mateso ya milele. Wengi wanadhani tajiri aliienda kuzimu na ombaomba(Lazaro) akaenda mbinguni. Lakini mstari wa 22 unasema yule ombaomba alikufa na akachukuliwa na malaika mpaka "kifuani mwa Ibrahimu." Je, tunapaswa kuamini "kifuani mwa Ibrahimu" kuwa ni mbinguni ambako Mungu anakaa? Hakika sivyo!

Wengine wanafikiri maneno haya yanaelezea tukio halisi lililowapata watu wawili. Ikiwa hiyo ilikuwa kweli, njia ya kwenda mbinguni ni kuwa ombaomba mwenye vidonda kwenye mwili wake. Lakini uchunguzi utaonyesha jinsi isivyofaa kuchukulia hii kama lugha halisi.

**Penye lango lake palikuwa na ombaomba mmoja aitwaye Lazaro, ana vidonda vingi:** Ombaomba huyu alikuwa amelala kwenye lango la nyumba ya tajiri na kutokana na simulizi, huu ulikuwa ni utaratibu wa kudumu. Wakati fulani tajiri alikuwa akipeleka chakula kutoka kwa meza yake kwenda kwa ombaomba. Lakini hebu fikiria juu ya hilo. Ni tajiri gani leo angeruhusu mpangilio wa aina hii kwenye lango

[1]Nukuu zote za Maandiko zimetoka katika *Toleo Jipya la* Biblia la Kimataifa isipokuwa kama imetambulishwa vinginevyo.

lake? Je, wewe ungeiruhusu? Na bado tajiri huyu anahesabiwa kuwa mbaya, mtu ambaye anapaswa kuteswa alipokufa.

**Hata mbwa walikuja na kulamba vidonda vyake:** Tunawaona ombaomba wametuzunguka pande zote, wengine bila miguu na mikono, wengine na majeraha. Lakini kwa hakika hakuna hata mmoja wao ambaye angeruhusu mbwa kulamba vidonda vyao! Itakuwa aibu kubwa! Kwa hivyo kile kinachosemwa juu ya ombaomba huenda hakijawahi kutokea.

**Nihurumie na umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake katika maji na aupoze ulimi wangu, kwa sababu ninateseka katika moto huu**: Hebu wazia mtu katika moto mkali na joto kali. Je, tone tu la maji kwenye ulimi lingeweza kuleta ahueni yoyote? Ikiwa mtu yeyote alikuwa katika moto, unaweza kuwa na hakika kwamba ombi lake moja lisingekuwa la kidole kilicholowa kugusa  ulimi wake.

Mara nyingi Bwana alinena kwa mifano: “*Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; hakusema nao neno lo lote pasipo kutumia mfano*” (Mathayo 13:34). Linganisha mwanzo wa kifungu hiki (Luka 16:19-31) na mifano mingine michache ya Yesu: “Palikuwa na mtu…” (Luka 15:11). “Palikuwa na mtu mmoja tajiri ambaye msimamizi wake …” (Luka 16:1). “Mtu mmoja mwenye cheo cha juu alikwenda nchi ya mbali…” (Luka 19:12). “Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu…” (Luka 20:9). Kwa hiyo, Yesu anapoanza kwa kusema, “Kulikuwa na mtu tajiri,” wasikilizaji wake walijua kwamba huo ulikuwa mfano. Sasa tutaangalia maana ya ishara zake.

**Tajiri Anawakilisha Tabaka (kundi)**

"Palikuwa na mtu mmoja tajiri, aliyevaa mavazi ya zambarau na kitani safi, akiishi maisha ya starehe kila siku" (Luka 16:19). Katika Luka 15:11, mfano wa tatu katika mfululizo huu wa mifano mitano,

mtu mmoja alikuwa na wana wawili, mmoja wao akiwa “mpotevu” na mwingine akionekana kuwa “mshikamanifu.” Wana wawili wanawakilisha tabaka mbili za watu. Katika mfano huu wa tano katika mfululizo huo, “tajiri” aliwakilisha taifa la Israel.

**Amevaa mavazi ya zambarau**: Zambarau ilikuwa rangi inayohusishwa na mamlaka ya kifalme. Yesu alipewa vazi la zambarau na kisha kwa dhihaka akaitwa “Mfalme wa Wayahudi” (Yohana 19:2,3). Taifa la Israeli lilikuwa na “ahadi za kifalme” za “kujivika” wenyewe: “*Sasa kama mkinitii kwa utimilifu na kulishika agano langu, ndipo mtakuwa milki yangu kutoka katika mataifa yote; mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani na taifa takatifu*” (Kutoka 19:5,6). “Kuvikwa mavazi ya zambarau” inawakilisha ahadi za ufalme za Mungu ambazo ilifunika taifa la Israel.

**Kitani nzuri** : Kitani kinawakilisha haki: "*Kitani nzuri huwakilisha matendo ya haki ya watakatifu*" (Ufunuo 19: 8). Haki ya Waisraeli haikuwa halisi bali ilitimizwa kupitia dhabihu za kila mwaka za siku ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zao: “*Hii itakuwa amri ya kudumu kwenu: Siku ya kumi ya mwezi wa saba mtajikana nafsi zenu, wala msifanye kazi yo yote, kwamba ni mzaliwa wa kwanza; mzaliwa au mgeni akaaye kati yenu, kwa maana siku hii upatanisho utafanywa kwa ajili yenu, ili kuwatakasa. Kisha, mbele za BWANA, mtakuwa safi na dhambi zenu zote. Ni sabato ya kustarehe kabisa, nanyi mtajikana nafsi zenu; ni amri ya kudumu*.” (Mambo ya Walawi 16:29-31). Dhabihu hizi kwa kawaida zilihalalisha Israel kuwaweza kumkaribia Mungu katika sala. “Walikuwa wamevikwa kitani nzuri” machoni pa Mungu kwa sababu dhambi zao zilifunikwa.

**Aliishi maisha ya starehe kila siku**: Neno la Mungu linafananishwa na chakula ambacho kinapaswa kuliwa: "*Maneno yako yalipokuja, niliyala*" (Yeremia 15:16). Ilikuwa Israel, peke yake kati ya mataifa, ndiyo iliyopendelewa na kubarikiwa kwa maneno mengi sana ya

Mungu: *"Zishikeni kwa uangalifu; kwa kuwa hii itaonesha hekima yenu na ufahamu wenu kwa mataifa. Ni taifa gani lingine lililo kuu hata kuwa na miungu yao karibu nao kama BWANA, Mungu wetu, alivyo karibu nasi kila tumwombapo? Na ni taifa gani lingine kubwa hata kuwa na amri na sheria za uadilifu kama kifungu hiki cha sheria ninachoweka mbele yenu leo? Je! kuna watu wengine waliosikia sauti ya Mungu ikizungumza kutoka katika moto kama ninyi mlivyosikia, nao wakaishi?"* (Kumbukumbu la Torati 4:6-8,33).

Hivyo "tajiri" alifananisha taifa la Israel ambalo lilipokea maneno mengi ya Mungu. Agano lote la Kale lenye maneno ya manabii, kuanzia Samweli hadi Malaki, lilitolewa kwao tu. Walifanya karamu ("waliishi kwa starehe") kila siku. Hivyo katika "picha hii" Yesu alifafanua taifa la Israel.

**Lazaro Anawakilisha Tabaka (kundi) Tofauti**

*"Mlangoni mwake palikuwa na ombaomba mmoja aitwaye Lazaro, ambaye ana vidonda vingi na akitamani kula kile kilichoanguka kutoka kwenye meza ya yule tajiri. Hata mbwa walikuja na kulamba vidonda vyake."* (Luka 16:20, 21) "Ombaomba" huyo anawakilisha watu wasio Wayahudi, watu wa mataifa.

**Ombaomba**: Watu wa Mataifa walikuwa maskini katika baraka za Mungu, kwa kweli hawakuwa na baraka hata kidogo! Kwa maana hiyo waliishi katika umasikini kabisa!

**ana vidonda vingi**: Hali ya dhambi miongoni mwa Mataifa haikutoa njia ya kutakasa na kupata upatanisho kwa ajili ya dhambi zao. "Vidonda" hivi vinawakilisha hali ya kutosamehewa ya dhambi ambayo walijikuta ndani yake.

**Langoni mwake** : "Nyumba" iliwakilisha hali ya upendeleo ya taifa la Israel. "Ukuta" wa nyumba hiyo ulikuwa ni Agano la Sheria: "*Kwa*

*maana yeye ndiye amani yetu, aliyewafanya hao wawili kuwa wamoja, akakibomoa ukuta wa uadui"* (Waefeso 2:14). "Lango" lilikuwa tohara (Mwanzo 17:12-14), ishara ya nje ambayo kwayo mtu alionyesha imani katika agano la Mungu pamoja nao. Watu wa Mataifa walikuwa nje ya "ukuta" na "lango" hilo pia.

**Makombo kutoka mezani**: Hizi zilikuwa baraka ndogo ndogo ambazo Mataifa walitafuta kama ilivyoonyeshwa wakati Yesu alipozungumza na mwanamke Mkanaani (Mathayo 15:25-28).

**Mbwa walilamba vidonda**: "Vidonda" vinawakilisha hali ya dhambi isiyosamehewa; "kulamba" vidonda kungewakilisha aina ya kitulizo au faraja. Inaeleza njia ambazo watu wa Mataifa wangetafuta faraja kutokana na dhambi zao. Mbwa ni mnyama najisi (Mambo ya Walawi 11:27). Hivyo maneno "mbwa walilamba vidonda vyake" yanaashiria njia chafu ambayo kwayo watu wa mataifa mengine walitafuta upatanisho wa dhambi kama vile kuabudu sanamu, ushirikina, imani upofu, dhabihu za watoto, ukahaba wa hekaluni, na kadhalika. Hii ndiyo ilikuwa hali ya watu wa mataifa mengine.

*"Wakati ukafika ambapo yule ombaomba alikufa na malaika wakamchukua mpaka kando ya Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa."* (Luka 16:22) Kitenzi "alikufa" humaanisha mwisho. Wote wawili "walikufa" katika maana ya kwamba kipindi cha upendeleo kwa Wayahudi kilichooneshwa wakati wa zama ya Kiyahudi kilifika mwisho. Vile vile kipindi cha kutopendelewa na Mataifa kiliisha wakati zama ya Injili ilipoanza.

**Lazaro**: Anawakilisha watu wa Mataifa waliokubali injili, ambao walikuja kuwa Wakristo, na kuingia katika kibali cha Mungu.

**Malaika walimbeba mpaka kifuani mwa Ibrahimu**: Malaika wanawakilisha wajumbe wa injili ndani ya kanisa la kwanza

waliotumwa kwa Mataifa. Hao ni pamoja na mtume Petro ambaye "alifungua mlango kwa Mataifa" katika nyumba ya Kornelio, mtume Paulo aliyekuwa mtume aliyechaguliwa hasa kwa Mataifa (Wagalatia 2:8 ), na wengine waliojishughulisha na kazi hii kama vile Barnaba, Tito; Sila, na Luka. "kifuani mwa Ibrahimu" ni sawa na kusema kwamba mtu alifanyika sehemu ya "watoto wa Ibrahimu": "*Fahamuni basi, ya kuwa **wale walioamini** ni watoto wa Ibrahimu*" (Wagalatia 3:7). Hivyo hawa wanakuwa warithi wa ahadi ya Ibrahimu (taz. Wagalatia 3:16,29).

**Tajiri pia alikufa na akazikwa** : kipindi cha neema cha Israeli (zama ya Kiyahudi) kiliisha na taifa "lilizikwa" kama lilivyotoweka, na kutokuwepo tena. Israeli ilikoma kuwa taifa baada ya mwaka wa 70 B.K

"*Katika kuzimu, mahali alipokuwa katika mateso, [yule tajiri] alitazama juu, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro karibu naye. Akamwita, Baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu, kwa maana ninateseka katika moto huu*". (Luka 16:23, 24) Hili laeleza hali ya taifa la Israel baada ya 70 BK walipotawanywa katika mataifa yote: "*Nilipoita, hawakusikia; hivyo watakaponiita, mimi sitasikiliza, asema Bwana wa majeshi. Nitawatawanya kwa upepo wa kisulisuli kati ya mataifa yote ambako walikuwa wageni.*" (Zekaria 7:13, 14) Hii ni picha ya wazi ya mateso yao.

**Mateso katika moto huu**: Moto ni ishara ya hukumu iliyokuja kwa Israeli mwanzoni wakati Yesu aliposema, "*Nyumba yenu mmeachiwa ukiwa*" (Mathayo 23:38). Hii ilikuwa mwaka 33 BK kabla tu ya kusulubishwa. Wale waliopaza sauti zao kusulubishwa kwake waliomba adhabu yao: "*Watu wote wakajibu, Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu*" (Mathayo 27:25). Mara nyingi hasira ya Bwana inaonyeshwa na moto: "*Nimeamua kuwakusanya mataifa, ili kukusanya falme na kumwaga ghadhabu yangu juu yao—hasira yangu yote kali.*

*Ulimwengu wote utateketezwa kwa moto wa hasira yangu yenye wivu."* (Sefania 3:8 )

**Alimwona Ibrahimu kwa mbali**: Israeli walitambua kuwa hawakuwa na kibali cha Mungu na katika mfano huu Ibrahimu alifananisha Mungu kama alivyofanya wakati alipomtoa mwanawe Isaka kwa hiari, picha ya Mungu akimtoa mwanawe wa pekee kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

**Lazaro kifuani mwake**: Hii inaeleza hali ya baraka ya upendeleo ambao Mungu aliwapa mataifa ya Wakristo wakati wa zama ya Injili.

**Umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake katika maji na aupoze ulimi wangu**: Hii inalinganishwa na maombi ya Wayahudi kwa mataifa ya Kikristo kuonyesha upendeleo mdogo kama vile kupata makazi, shule, na mahali pa masinagogi. Lakini hili lilikuwa jibu: "*Ibrahimu akamjibu, Mwanangu, kumbuka ya kuwa ulipokea mema yako katika maisha yako, na Lazaro alipata mabaya, lakini sasa anafarijiwa hapa, na wewe unateseka. Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale wanaotaka kutoka huku kwenda kwenu wasiweze, wala mtu kutoka huko asiweze kuvuka kuja kwetu."*

Ingawa Abrahamu anazungumza, hii ni picha ya Mungu akizungumza! Mungu anazungumza kupitia Neno lake ambalo linaweka wazi zama ya Kiyahudi ilikuwa ni wakati wa baraka (neema) kwa Wayahudi na kutopendelewa kwa Mataifa. Katika zama ya Injili ni kinyume chake: baraka ni kwa Mataifa wanaoamini na mateso(kutopendelewa) ni sehemu ya Wayahudi waliopofushwa. "shimo kubwa" ni utengano kati ya Uyahudi na Ukristo.

**Pengo(shimo) kubwa limewekwa**: Kizuizi hiki kilikuwa ni hali ya kutoamini kwa Wayahudi kumpokea Yesu. Hivyo hawakuweza kuvuka upande wa baraka kwa kumpokea Yesu.

**Wale wanaotaka kutoka huku [upande wa Ibrahimu] kwenda kwenu wasiweze**: Ilikuwa haiwezekani kuachilia taifa la Israel kutoka katika utumwa wa sheria kwa mahubiri ya Kikristo: "*Enyi Wagalatia msio na akili! Nani amewaloga? Mbele ya macho yenu Yesu Kristo alionyeshwa waziwazi kuwa amesulibiwa*." (Wagalatia 3:1)

**wala mtu yeyote kutoka huko [upande wa tajiri] asiweze kuvuka kuja kwetu**: Wayahudi walikuwa wa zama nyingine. Walimfuata Musa na torati na kumkataa Yesu; hata hawakumtambua: "*Tunajua kwamba Mungu alisema na Musa, lakini kuhusu mtu huyu hata hatujui alikotoka*" (Yohana 9:29). Hili lilikuwa pengo (shimo) pana kweli!

Kisha tajiri huyo anaomba jambo lingine: "*Nakusihi, baba, umtume Lazaro nyumbani kwa baba yangu, kwa maana ninao ndugu watano. Na awaonye, ili wao pia wasije mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akajibu, Wana Musa na Manabii; waache wawasikilize. Akasema, la, baba Ibrahimu, lakini ikiwa mtu kutoka kwa wafu akiwaendea, watatubu. Akamwambia, wasipowasikiliza Musa na manabii, hawatasadiki hata akifufuka mtu katika wafu*." Hii inaonyesha hali ya bila msaada ya taifa la Israel wakati wa zama ya Injili.

**Ndugu watano**: Kwa pamoja hawa ni taifa la "kabila kumi" la Israel huku tajiri akiwakilisha "taifa la kabila mbili la Yuda. "Ikawa Rehoboamu alipofika Jerusalem, akaikusanya nyumba ya Yuda na Benyamini, watu mia na themanini elfu, wapiganaji, ili kupigana na nyumba ya Israel na kuurudisha tena ufalme kwa Rehoboamu mwana wa Sulemani. Lakini neno hili la BWANA likamjia Shemaya mtu wa Mungu, kusema, Mwambie Rehoboamu, mwana wa Sulemani, mfalme wa Yuda, na Waisraeli wote katika Yuda na Benyamini, Bwana asema hivi, Msipande kupigana na ndugu zenu. Nendeni nyumbani, kila mmoja wenu, kwa maana hili ni kazi yangu." (2 Mambo ya Nyakati 11:1-4 )

Baada ya kifo cha Mfalme Sulemani taifa la Israel lenye kabila kumi na mbili liligawanyika sehemu mbili: makabila mawili ya Yuda na Benyamini yakawa taifa la Yuda na makabila kumi yaliyobaki yakawa taifa la Israel. Kwa hiyo , ikiwa "tajiri" katika mfano huu anawakilisha taifa la makabila mawili la Yuda, basi ndugu watano lazima wanawakilisha taifa la makabila kumi la Israeli.

**Musa na Manabii** : Haya ni maandishi ya Agano la Kale pamoja na maelezo yake ya jinsi ambavyo Masihi lazima kwanza ateseke na kufa kabla ya kupata utukufu na ufalme (taz. Isaya 53, Zaburi 22, nk.). Wayahudi hawakuweza kutambua kipengele hiki cha Masihi wao na hivyo hawakuweza kumtambua Yesu.


**Aliyefufuka kutoka kwa wafu**: Rejea hii haimhusu **Yesu**! Sio lugha halisi. anayerejelewa kuwa aliyekufa na kisha kufufuka kutoka kwa wafu anaelezwa na mtume Paulo: "*Ninyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu*" (Waefeso 2:1, KJV). Hawa ni Wakristo, na hasa Wakristo wa Mataifa ambao "wamefufuka" kutoka katika hali ya "wafu" waliyokuwanayo, na ambayo ulimwengu bado upo ndani yake (Luka 9:60). Hakuna juhudi za Kikristo za kuhubiri injili zinazoweza kuokoa au kubadilisha taifa la Israel. Lakini hiyo haimaanishi kuwa taifa la Israeli limepotea. La hasha!

"*Ndugu zangu, sipendi mkose kuijua siri hiyo, ili msije mkajivuna; ugumu umewapata Israeli kwa sehemu, hata hesabu kamili ya Mataifa itakapotimia; na hivyo Israeli wote wataokolewa, kama ilivyoandikwa: Mkombozi atatoka Sayuni; ataondoka kutokumcha Mungu katika Yakobo*" (Warumi 11:25,26). Israel wote "wataokolewa"! Wokovu wao utafuata wokovu wa Kanisa. Mpango wa Mungu una wokovu mbili: moja ni wokovu wa mbinguni kwa kanisa, na mwingine ni wokovu wa duniani kwa Israeli na ulimwengu wote wa wanadamu.

Mfano huu unaelezea tabaka mbili na hali yao katika zama mbili. Yesu aliposema maneno haya aliishi wakati wa kufungwa kwa zama ya Kiyahudi na kufunguliwa kwa zama ya Injili.

Tafadhali tambua kwamba ingawa tumejadili mfano/fumbo hili kama sehemu ya somo letu la nafsi, fumbo hili, hata hivyo, halirejelei habari ya nafsi hata kidogo! Ukweli uko wazi: "*Nafsi itendayo dhambi ndiyo itakayokufa*" (Ezekieli 18:4). Nafsi zote zinakufa!

**-Amina-**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***